TANGAZO LA SERIKALI Na. 281 La Tarehe 19/3/2021

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA MAMLAKA ZA WILAYA.
[SURA YA 287]

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya kifungu cha 153).*

SHERIA NDOGO YA UDHIBITI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA MWAKA, 2021

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ya Mwaka 2021.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-

“Afisa Mifugo” maana yake ni Afisa mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya au mtumishi yeyote wa Halmashauri mtaalam wa mifugo;

Afisa Mwidhiniwa” maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa kusimamia Sheria Ndogo hii;

“eneo la Mifugo” maana yake ni eneo lililotengwa kwa ajili ya kulishia na kufugia mifugo;

“eneo la kilimo” maana yake ni eneo lililotengwa kwa ajili ya kilimo tu;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya;

“kibali” maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

“mifugo” maana yake ni wanyama wote wafugwao na ambao hutegemea majani kama chakula chao kikuu;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya;

## SEHEMU YA PILI.
## ENEO LA KUFUGIA.

Eneo la kufugia

3.- (1) kila serikali ya kijiji itatenga eneo la kufugia na kuchungia mifugo kwa kuzingatia uwiano kati ya idadi ya mifugo na eneo lililotengwa.

(2) Serikali ya kijiji itawajibika kuhakikisha maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji yanatunzwa.

Marufuku ya mifugo

4. (1) Itakuwa ni marufuku kwa maeneo yafuatayo kuwa sehemu ya eneo la kufugia mifugo:-

(a) Maeneo ya vyanzo vya maji;
(b) Maeneo ya makazi ya watu;
(c) Maeneo yaliyotengwa kwa kilimo;
(d) Maeneo tengefu ya Serikali;

(2)Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hii kwa Mkulima yeyote kufanya shughuli za kilimo katika eneo lilitengwa kwa ajili ya mifugo.

## SEHEMU YA TATU
## IDADI YA MIFUGO

Idadi ya mifugo

5.- (1) Kila mfugaji atatakiwa kuwa na idadi ya mifugo inayowiana na eneo lililotengwa kwa ajili ya kufugia.

(2) Kamati ya mifugo na mazingira, mifugo na ulinzi ya kijiji itakuwa na wajibu wa kukagua idadi ya mifugo kwa kila mfugaji, zoezi hili litakuwa kila mwezi.

(3) Tarehe ya ukaguzi ni sharti ijulikane kwa wananchi wote.

(4) Taarifa ya ukaguzi sharti iwasilishwe kwenye

ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji(W) mara baada ya ukaguzi.

SEHEMU YA NNE.
MIFUGO MIPYA NDANI YA WILAYA.

Zuio

6.- (1) Ni marufuku kuingiza mifugo mipya ndani ya wilaya isipokuwa kwa kibali halali kilichotolewa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Sheria Ndogo hii pamoja na Sheria zingine za nchi hii.

(2) Kamati ya Mazingira, Mifugo, na Ulinzi za kijiji zitakuwa na jukumu la kuhakikisha mifugo mipya haingii ndani ya kijiji bila kibali maalum.

(3) Itakuwa ni wajibu kwa kila Mwananchi kuhakikisha anatoa taarifa kwenye ngazi husika endapo ataona mifugo mipya inaingizwa kinyemela ndani ya wilaya au kijiji.

(4) Ni marufuku kwa mfugaji kufugia mifugo yake kama yeye si mkazi wa wilaya hii au kijiji husika.

Utaratibu wa kuingiza mifugo mipya

7.- (1) Mifugo mipya ndani ya wilaya au kijiji itaingizwa kwa kibali maalumu.

(2) Kibali cha kuingiza mifugo mipya ndani ya Wilaya kitatolewa na Halmashauri baada ya kujiridhisha na uhalali na usalama wa mifugo hiyo.

(3) Kibali cha kuingiza mifugo mipya ndani ya kijiji kutoka kijiji kingine au sehemu nyingine ndani ya Wilaya kitatolewa na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.

(4) Mfugaji yeyote hataruhusiwa kuhamia ndani ya Wilaya au kijiji kama atakuwa hana kibali cha uhamisho.

(5) Vibali vitatolewa kufuatia ombi maalum la

kimaandishi kutoka kwa mfugaji.

(6) Ombi la Mifugo kuhamia ndani ya Kijiji sharti lijadiliwe na kuafikiwa au kukataliwa na Serikali ya kijiji ambako Mifugo inataka kuhamia.

(7) Ombi la uhamisho likishakubaliwa na kijiji, Serikali ya kijiji itaandaa muktasari ukiwa na ajenda ya kukubali ombi la mfugaji kuhamia kijijini kwao na kuupeleka kwenye Halmashauri.

(8) Mamlaka ya kutoa kibali inaweza kukataa kutoa kibali hata kama Kijiji au kata anakotoka mfugaji amekubaliwa.

MAKOSA NA ADHABU

Makosa

8. Mtu yeyote atakaenda kinyume na Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Adhabu

9. Mtu yeyote atakaekutwa na kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatumikia kifungo cha miezi kumi na miwili jela au atalipa faini isiyopungua shilingi laki tatu au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki moja endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hii.

JEDWALI

*(*Limetungwa chini ya kifungu cha 10)

KUFILILISHA KOSA

Mimi…………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, kwamba mnamo tarehe ………mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ya mwaka 2021.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halamashauri ya Wilaya ya Chunya, nipo tayari kulipa kiasi ninachodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……………………………… ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo…………………………………….

Saini………………………………………Tarehe……………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imebandikwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 30/6/2020:-

SOPHIA JUMA KUMBULI,
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Chunya*

MHE. BOSCO SAID MWANGINDE,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Chunya*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
22 Februari, 2021

SELEMANI SAID JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR- Tamisemi*